



Yesu Alituamuru Tushiriki Injili

Baada ya kufufuka, Yesu aliwatembelea Mitume Wake. Aliwapatia samaki na mkate wale.

Yesu alimwuliza Petero, “Je, wanipenda?”

Petro alisema ndiyo. Kisha Yesu akasema “Lisha kondoo wangu.”

Yesu alimwuliza Petro mara mbili zaidi. “Je, wanipenda?”

Mara zote Petro alisema ndiyo. Na mara zote Yesu alisema, “Lisha kondoo wangu.”

Petro alijifunza kwamba Yesu alikuwa akimwamuru ashiriki injili. Yesu ni Mchungaji wetu na sisi ni kondoo Wake.

Tunaweza kuonesha upendo wetu kwa Yesu kwa kuwasaidia wengine wajifunze kuhusu Yeye na wamfuata Yeye. ●

Unaweza kusoma hadithi hii katika Yohana 21:15-17.



Ondoa ukurasa huu na ukunje katika nusu mbili zinazolingana. Kisha inua picha juu wakati ukisimulia hadithi.

